Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya

Mamlaka, Majukumu na Uwajibikaji

Jalida la Polisi Shirikishi

MEI, 2017
HAKI NA USALAMA
http://hakinausalama.org/

Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya

Mamlaka, Majukumu na Uwajibikaji

Jalida la Polisi Shirikishi

MAY 2017
HAKI NA USALAMA
http://hakinausalama.org/

Kuhusu Jukwaa la Haki na Usalama

Jukwaa la Haki na Usalama lilianzishwa Desemba mwaka 2012. Jukwaa linahamasisha uwepo wa mfumo wa demokrasia wa utendaji wa Jeshi la Polisi. Hivi sasa jukwaa hili, linajumuisha wadau mbalimbali na kutoa fursa ya kujadili marekebisho katika Jeshi la Polisi.

Wanachama wa jukwaa hili kwa sasa ni pamoja na Chama Cha Wanasheria Tanganyika (TLS); Asasi ya Haki za Binadamu ya Jumuiya ya Madola (CHRI); Jukwaa la Adhama ya Watoto (CDF); Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC); Shirika la Kitaifa la Msaada wa Kisheria (NOLA); Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC); Kituo cha Msaada wa Kisheria cha Wanawake (WLAC); Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA); Chama cha Vijana Tanzania (TYVA); Shirika la Wanawake la Hatua za Kufikia Maendeleo ya Kiuchumi (WATED); Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo la Afrika (WILDAF) na Mtandao wa Afrika wa Kuzuia na Kulinda Unyanyasaji na Utelekezaji wa Watoto (ANPPCAN).

Washirika wengine wa jukwaa hili ni pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania (TPF); Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG); Open Society Initiative for East Africa (OSIEA) na Taasisi ya Kimataifa ya Hanns Seidel (HSF).

SHUKRANI

Kufanikiwa kwa kijaridi hiki ni kutokana na mchango muhimu na nguvu kazi jumuishi za watu mbalimbali kutoka mashirika kadha wa kadha.

Kazi ya kutafiti, kukusanya na kuhariri, ulifanywa na Asasi ya Haki za Binadamu ya Jumuiya ya Madola (CHRI) na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora chini ya uratibu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Shukrani za dhati kwa wote walitoa muda na mchango wao, ikiwa ni pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania, Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania na wanachama wa Jukwaa la Haki na Usalama katika zoezi la utafiti na uhakiki wa jarida hili.

Kwa dhati, Jukwaa la Haki na Usalama linashukuru na kuthamini fadhila iliyotolewa na Open Society Initiative For Eastern Afrika (OSIEA) ili kukamilisha jarida hili.

YALIYOMO

Kuhusu jukwaa la haki na usalama ii
Shukrani iii
Utangulizi 1
1. Uchambuzi wa kina wa muundo wa kisheria wa kamati za ulinzi na usalama za wilaya, sheria ya baraza la ulinzi na usalama wa taifa, 2010 3
1.1. Muundo wa baraza na wajumbe 3
1.2. Majukumu na kazi za kamati 6
1.3. Sheria zingine 10
2. Uchambuzi wa kina wa utendaji wa kamati za ulinzi na usalama za wilaya 12
2.1. Kutekeleza majukumu ya kikatiba 12
2.2. Utendaji wa siku hadi siku 16
2.3. Ukweli na uwazi kwa umma 17
2.4. Kushughulikia malalamiko na ripoti kutoka kwa umma 19
3. Uwezo wa kamati za ulinzi na usalama za wilaya kiuwajibishaji na kiusimamizi 22
Rejea 28
Kiambatisho i: dodoso kwa kamati za ulinzi na usalama za wilaya 29
Kielelezo ii: sura za wilaya 36

UTANGULIZI

> "*Matendo ya maafisa wanaosimamia utekelezaji wa sheria ni lazima wawajibike kwa umma, iwe kupitia bodi, wizara, mahakama, ofisi ya mwendesha mashtaka, msimamiza wa sheria wa jamii (Ombudsman), kamati ya wananchi au muundo wowote wa aina hiyo, au taasisi yeyote*" – Umoja wa Mataifa, Mwongozo wa Maadili kwa Maafisa Watekelezaji wa Sheria, Maelezo ya Awali.

Tanzania imeweka mfumo ambao masuala ya ulinzi na usalama yanajadiliwa kupitia kamati za ulinzi na usalama kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa. Kutokana na mabadiliko na maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na pia ongezeko la matukio ya makosa ya jinai na mifumo ya haki duniani jitihada mbalimbali zinafanyika ili kufanya mageuzi katika kamati za aina hii. Hivyo, Tanzania kama nchi zingine za jumuiya ya madola inapaswa kubadili sheria zake za usalama ili ziendane na viwango vya kimataifa vya ulinzi na usalama. Hili litarahisisha ushiriki wa wananchi katika masuala ya usalama na kuimarisha mfumo wa kulinda haki za binadamu.

Kuwashirikisha wananchi katika hatua za usalama kumejengwa katika misingi ya haki na usawa, uwajibikaji, uwazi, ushirikishwaji, kuheshimu utofauti wa watu, kukubali kutokukubaliana, kulinda haki za kila mtu na makundi, pia kuhamasisha umuhimu wao kwa jamii.[1] Nchi nyingi hususan zile zinazofanya mageuzi ya kidemokrasia zinatumia mfumo huu wa kiusalama.

Hili ni andiko la tatu kutoka kwa wanachama wa Jukwaa la Haki na Usalama ambao wanawiwa kuchangia na kushiriki katika zoezi na jitihada zinazoendelea za kutekeleza mfumo wa kidemokrasia wa polisi nchini Tanzania. Hivyo, andiko hili limechambua kwa kina uwezo wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kuwa ngazi za uwajibikaji wa polisi, na mabadiliko yanayopaswa kufanywa yenye dhima ya kuboresha na kutekeleza jukumu hilo.

1 "Police Accountability: Too Important to Neglect, too Urgent to Delay". Commonwealth Human Rights Initiative, 2005, p.12;

Mapendekezo yaliyotolewa yametokana na uchambuzi wa sera na sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa (NSC Act) ya 2010 na usaili wa kamati nane za Ulinzi na Usalama za Wilaya uliofanyika kupitia dodoso (rejea Kiambatisho I). Kamati zilizosahiliwa ni kutoka wilaya zifuatazo: Kibiti; Lindi; Nyamagana; Rufiji (Utete); Uyui; Tabora; Nzega; and Kaliua (rejea kiambatisho II). Maswali ya dodoso yalisambazwa na kusimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa niaba ya jukwaa. Tume iliwasilisha maombi ya usaili kwa Wakuu wa Wilaya 20 ambapo Wakuu wa Wilaya 11 waliridhia kushiriki na Wakuu wa Wilaya wanane tu ndio walijaza na kujibu maswali ya dodoso. Tume inaamini kuwa muitikio huu mdogo umechangiwa na imani kuwa mambo ya kiusalama ni nyeti na siri, hivyo hayapaswi kujadiliwa na mtu yeyote nje ya mamlaka za kiusalama.

Chapisho hili limegawanyika katika sehemu kuu tatu, kwanza, linachambua Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa, 2010 kwa kuainisha majukumu ya kiusalama ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, na kubainisha iwapo mipaka ya majukumu yao inaruhusu kusimamia polisi. Pili, linaangalia kwa kina ni kwa kiasi gani majukumu ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya hudhihirika kiutendaji, ikijumuisha masuala ya kiutendaji (namna gani kazi zao zimepangiliwa) na ni masula yapi kamati inashughulikia na kwa namna ipi. Sehemu ya tatu imejengwa kutokana na masuala mawili yaliyoelezwa hapo juu ambayo hupelekea kueleza kuwa kamati hizi zinaweza kuwawajibisha na kusimamia utendaji wa polisi kwa umma na hivyo kupendekeza kubadilishwa kwa sera ili kujumuisha jukumu hili.

1. Uchambuzi wa Kina wa Muundo wa Kisheria wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, Sheria ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, 2010

Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zimeanzishwa chini ya Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa, 2010 (NSC Act) kama ngazi ya chini kabisa kati ya tatu zinazoshugulika na masuala ya ulinzi. Ngazi nyingine mbili ni Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa (RSCs) na Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa. Kwa sheria hii hakuna kamati za ulinzi na usalama katika ngazi ya kata na kijiji.

Utangulizi wa Sheria hii unaeleza kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zimeanzishwa ili "kusimamia na kuratibu masula ya kiusalama wa taifa" na muhimu zaidi "kuweka mfumo maalum wa wananchi, taasisi za umma na binafsi kushiriki kikamilifu katika masuala ya ulinzi na usalama wa nchi.[2] Lengo la kuhusisha wadau wengi katika "kushiriki" na "kuchangia"sera za masuala ya kiusalama kwa kiasi kikubwa huendana na misingi ya utawala wa kidemokrasia na utendaji wa kidemokrasia kwa polisi. Japokuwa, kama itakavyooneshwa katika chapisho hili, kuna utofauti mkubwa kati ya malengo ya ushirikishwaji na maelezo ya vifungu vya sheria.

1.1. Muundo wa Baraza na wajumbe

Kifungu cha 4 cha Sheria kilichoanzisha Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa kinataja wajumbe kuwa ni, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (Mwenyekiti wa Bazara), Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri Mkuu, na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.[3] Katibu wa bazara la usalama anakuwa ni Katibu Mkuu Kiongozi.[4] Baraza la Usalama wa Taifa linaweza kuwaalika watu wengine katika kikao ili kutoa ushauri wa kitaalam.[5]

2 Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama, Usuli
3 *Id*, Kf. 4(1);
4 *Id*, Kf. 4(2);
5 *Id*, Kf. 4(4);

Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa linasaidiwa na sekretarieti inayojuisha

- Katibu Mkuu Kiongozi (Mkuu na Mratibu wa sekretarieti);
- Waratibu wasaidizi wawili kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania;
- Waratibu wasaidizi wawili kutoka Usalama wa Taifa;
- Mratibu msaidizi mmoja kutoka Jeshi la Polisi;
- Mratibu msaidizi mmoja kutoka Idara ya Uhamiaji;
- Mratibu msaidizi mmoja kutoka Jeshi la Magereza Tanzania;
- Mratibu msaidizi mmoja kutoka Chuo cha magereza Zanzibar.[6]

Kwa kuangalia aina ya wajumbe wa sekretarieti iliyoainishwa hapa juu ni dhahiri inatoa mwongozo wa masuala yanayopaswa kupelekwa kwenye Baraza la Usalama wa Taifa kulingana na majukumu yao. Hivyo, hawa hujumuisha, Jeshi la Wananchi, Usalama wa Taifa, Polisi, Uhamiaji, Watekeleza sheria na Jeshi la Magereza. Hili linaonyesha ufinyu wa uelewa kuhusu usalama, kwa sababu maeneo mengine (kama usalama na upatikanaji wa chakula, usalama wa raia, or usalama wa masuala ya kijinsia) hayajawakilishwa.

Kwa sababu majukumu ya Sekretarieti ya Bazara la Ulinzi na Usalama wa Taifa kwa kiasi kikubwa yanafanana na yale ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kumekuwa na msuguano wa kimajukumu baina ya kamati ya Wilaya na Mikoa. Hii ni tofauti na Baraza la Usalama wa Taifa linalosaidiwa na Sekretarieti. Hivyo kufanya kamati za Wilaya na Mikoa kuwa za matukio maalum zaidi kuliko kuwa na majukumu ya kudumu ya kiusalama.

6 Zanzibari analogue of Tanzania Prisons Service; Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama, 2010.

Wajumbe wa Kamati ya Mkoa[7]	Wajumbe wa Kamati ya Wilaya[8]
• Mkuu wa Mkoa • Katibu Tawala wa Mkoa • Kamanda wa Polisi wa Mkoa • Kamanda Mkuu wa Vikosi vya JWT katika Mkoa • Afisa Usalama Mkuu wa Mkoa • Afisa Uhamiaji Mkuu wa Mkoa • Mshauri wa Jeshi wa Mkoa • Afisa Magereza Mkuu wa Mkoa	• Mkuu wa Wilaya • Katibu Tawala wa Wilaya • Kamanda wa Polisi wa Wilaya • Kamanda Mkuu wa Vikosi vya JWT katika Wilaya • Afisa Usalama Mkuu wa Wilaya • Afisa Uhamiaji Mkuu wa Wilaya • Mshauri wa Jeshi wa Wilaya • Afisa Magereza Mkuu wa Wilaya

Hakuna hata mjumbe mmoja wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya anayechaguliwa kidemokrasia. Wajumbe kisheria katika kamati hizi kwa upekee ni sehemu ya serikali au wateule wa serikali na ambao wanawajibika kwa serikali. Muundo huu unaleta ugumu kwa wananchi kushiriki na kujadiliana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa. Hivyo, kuna umuhimu wa kamati hizi kuwajibika kwa jamii husika na si kwa mamlaka za uteuzi upewe kipaumbele ili kuondoa changamoto hii.

Kwa kiasi suala la demokrasia limezingatiwa kwani Baraza la Usalama wa Taifa, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zinaweza kumwalika mtu yeyote katika vikao vyake "kwaajili ya kutoa ushahidi juu ya suala linalojadiliwa katika kikao". [9] Mamlaka haya hutumika zaidi katika Kamati ya Wilaya kama inavyoelezwa katika kifungu nambari mbili cha Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa.

Ushiriki wa umma umeelezewa zaidi kwenye majukumu yalitolewa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya ya "kuwa na

7 *Id*, Kf. 8(2);
8 *Id*, Kf. 10(1);
9 *Id*, Kf. 4(4), 8(3) na 10(2);

mfumo utakao wezesha ushiriki wa watu binafsi, taasisi za umma na binafsi kutoa na kuwasilisha taarifa zinazohusu masuala ya usalama wa taifa".[10] Mfumo huu ni muhimu sana katika kuhakikisha uwajibikaji kwa sababu umeeleza namna, japokuwa kwa ujumla sana, wa kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa wananchi/umma. Hivyo, hili hutengeneza mazingira ya kisheria kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kusimamia vyombo vya usalama kama polisi, jeshi na makampuni binafsi ya ulinzi kutekeleza majuku yao.

1.2. Majukumu na kazi za kamati

Majukumu yanayotekelezwa kisheria na Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya, huwa katika kuheshimu tange, kama ilivyoainishwa awali katika muundo na wajumbe wake.

Kwa mujibu wa Ibara ya 34(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, ulinzi na usalama ni Masuala ya Muungano,[11] mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu Masula ya Muungano yatakuwa chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano". Hivyo, ndiyo sababu Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa lilianzishwa "kama chombo kikuu cha kumshauri Rais kuhusu masuala ya usalama".[12] Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa lina kazi kubwa tano:[13]

- Kuunda, kuanzisha na kusimamia misingi mikuu ya usalama wa taifa kwaajili ya kulinda na kupigania maslahi ya taifa;
- Kufanya mapitio ya sera za ulinzi, usalama, masuala ya kimataifa na sera zingine zinazohusiana na usalama wa taifa katika muktadha ulipo kitaifa na kimataifa;
- Kutathmini, kwa muda mfupi na mrefu, hali ya usalama wa

10 *Id*, s. 14(3);
11 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2, 1977, Jedwali la 1, Kifungu 3;
12 Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama ya 2010, Kf. 5(1);
13 *Id*, Kf. 5(2);

taifa na kupendekeza hatua stahiki kuchukuliwa;

- Kupokea na kuchambua ripoti ya hali ya vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi na idara za serikali pia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na kutoa maelekezo sahihi; na
- Kufanya kazi zingine kama itakavyoelekezwa na Rais.

Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa kisheria linaonekana kuwa sehemu kubwa ya kazi zake ni kusimamia sera katika ngazi ya taifa. Iwapo litashughulika na masuala ya ulinzi na usalama katika ngazi zingine huwa ni "kutoa maelekezo" na hutolewa kulingana na taarifa zilizotolewa na kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya. Kwa muktadha huu, kwa sababu Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania anayo mamlaka ya kutoa maelekezo kwa Baraza la Ulinzi na Usalama, inawezekana baraza likawa na mamlaka makubwa ambayo hayakuainishwa katika sheria.

Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa[3]	Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya[4]
• Kupokea na kuchambua ripoti za usalama kutoka kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, vyombo vya ulinzi na usalama na kuchukua hatua stahiki; • Kuandaa ripoti ya tathmini kuhusu ya hali ya ulinzi na usalama na kuwasilisha kwa mamlaka husaka ndani ya mkoa; • Kupanga, kuratibu, na kutoa maelekezo ya namna ya kushughulika na dharura, makosa makubwa na matukie mengine yanayoweza kuaathiri utulivu na amani katika mkoa;	• Kuandaa mipango na mikakati ya ulinzi na usalama na kufutilia utekelezaji wake; • Kuandaa ripoti za tathmini za hali ya ulinzi na usalama katika wilaya na kuziwasilisha kwa katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa • Kupanga, kuratibu, na kutoa maelekezo ya namna ya kushughulika na dharura, makosa makubwa na matukio mengine yanayoweza kuaathiri utulivu na amani katika wilaya;

14 *Id*, Kf. 9;
15 *Id*, Kf. 11;

- Kubainisha na kutambua masuala ya kijamii na kiutawala ndani ya mkoa yanayoweza kuhatarisha usalama na kushauri mamlaka husika hatua za kuchukua;
- Kupokea maombi ya uraia na kumshauri waziri husika;
- Kupokea maombi ya umiliki wa silaha na vilipuzi na kufanya maamuzi kulingana na sheria zilizopo;
- Kutathmini na kufuatilia hali ya akiba ya bidhaa za kimkakati, (Chakula, madawa, na mafuta) na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kwa hatua zaidi;
- Kufanya kazi zingine kama itakavyo elekezwa na mamlaka husika.

- Kubainisha na kutambua masuala ya kijamii na kiutawala ndani ya wilaya yanayoweza kuhatarisha usalama na kushauri mamlaka husika hatua za kuchukua;
- Kupokea maombi ya uraia na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa;
- Kupokea maombi ya umiliki wa silaha na vilipuzi na kufanya maamuzi kulingana na sheria zilizopo au kuishauri Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa;
- Kutathmini na kufuatilia hali ya akiba ya bidhaa za kimkakati, (Chakual, madawa, na mafuta) na kutoa taarifa kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa hatua zaidi;
- Kufanya kazi zingine kama itakavyo elekezwa na mamlaka husika.

Kwa mujibu wa majukuma haya, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zimejikita zaidi katika kutatua matatizo yanayojitokeza katika maeneo yao. Kamati hizi hufuatilia hali ya usalama katika maeneo yao, huandaa mikakati ya kutatua matatizo na kutoa taarifa kwa mamlaka husika. Katika ngazi ya chini kabisa ya mfumo wa kuratibu usalama kisheria, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ndiyo ziko katika nafasi nzuri ya kutambua tatizo, kutoa msaada wa kiulinzi na kushughulika na kadhia iliyosababishwa kwa jamii.

Majukumu yaliainishwa hapo juu yanaonyesha umuhimu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama za Wilaya (na za Mikoa kwa kiasi fulani) kutoa ripoti za ulinzi na usalama ambazo huwasilishwa kila robo mwaka " kulingana na utaratibu wa mipaka ya kiutawala kijogorafia iliyowekwa".[16] Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa, na kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zinaweza kupokea taarifa za hali ya usalama, ambazo zinaonekana ni muhimu kwaajili ya "Ulinzi na Usalama, kutoka katika kikundi cha watu, jamii, au Umma kwa ujumla" [17] na kutoka kwa taasisi za umma na binafsi.

Kimsingi majukumu ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya ni mapana na yanajumuisha masuala mengine ambayo hayakuelezewa hapo juu. Hivyo, kuna utofauti mkubwa kati ya majukumu na muundo wa kamati, kwani wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya hawana uwezo au weledi wa kushughulikia masuala yote katika mamlaka peke yao. Hili hupelekea kamati hizi kutoa mialiko kwa wataalamu kuhudhuria vikao vya kamati ili kutoa maelezo ya kitaalam kwa suala husika na wakati mwingine huenda mbali zaidi kwa kuwataka wawe wajumbe wakudumu.

Kwa kuzingatia majukumu na kazi nyingi zinazokabili Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya, Sheria inaruhusu uanzishwaji wa kamati ndogo, "pale inapohitajika ili kutekeleza majukumu au kazi mahususi".[18] Katika mkutadha huo huo, Baraza la ulinzi na Usalama wa Taifa linaweza kuunda kamati ndogo.[19]

16 *Id*, Kf. 14(1);
17 *Id*, Kf. 14(2);
18 *Id*, ss. 8(4) na 10(3);
19 *Id*, Kf. 4(5);

1.3. Sheria Zingine

Kutokana na kuwa na kipengele cha usiri katika Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa kumewekwa ukomo wa wajumbe katika baraza. Sheria hairuhusu Baraza la Usalama la Taifa, kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya kutoa taarifa, mikakati, hatua za kiutawala za kiusalama kwa Bunge au umma. Kinyuma chake inabainisha adhabu kwa mjumbe yeyote wa kamati ambaye "anayetoa taarifa yeyote aliyoipata kutokana na yeye kuwa mjumbe wa kamati".[20] Pamoja na kuwa usiri unahitajika katika masuala ya ulinzi na usalama, kipengele hiki kimewekwa kiujumla mno, hivyo kuweka uhatari katika matumizi yake. Kipengele hiki kinakinzana na Sheria ya Kupata Taarifa ya 2015 (ATI Act) ambayo inaruhusu utoaji wa taarifa isipokuwa zile zilizozuiliwa chini ya kifungu cha 6(2). Taarifa zilizozuiliwa katika kipengele hiki zimeainishwa vizuri na kutoa maelekezo mazuri kwa mamlaka kuliko ile ya Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa inayozuia "taarifa yoyote".

Taarifa zinazohusu usalama wa taifa chini ya sheria ya Haki ya kupata Taarifa ATI Act, 2015[21]

"Taarifa zinazohusisha usalama wa taifa ni

a) Mikakati ya Kijeshi, mafunzo, uwezo, ukubwa au oparesheni;
b) Taarifa ya serikali kwa mataifa mengine zenye athari kwa usalama wa taifa;
c) Kazi na oparesheni za kiusalama, vyanzo au uwezo wa kitaarifa, mbinu za kijeshi au mbinu za kubaini mitego;
d) Mahusiano ya nje au kazi za kigeni;
e) Masuala ya kiuchumi, kisayansi ama teknolojia yanayohusisha usalama wa taifa; au
f) Uduni au uwezo wa mifumo, miundombinu, miradi, mipango au oparesheni zinazohusiha usalama wa taifa".

20. *Id*, Kf. 12;
21 Sheria ya Kupata Taarifa ya 2015, Kf. 6(3);

Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa haijatoa mwanya wa kutungwa kwa kanuni zitakazo saidia utekelezaji wake hii husababisha changamoto kwa wadau wanaoitekeleza. Hivyo, hakuna kanuni iliyotungwa na kutolewa kwa sheria hii. Kanuni hizo zingeeleza kwa ufasaha kazi za kamati, mpangilio wa vikao, utunzaji wa kumbukumbu, hatua za malalamiko, na kufafanua namna ya kutunza siri. Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya wameeleza hili kama changamoto (rejea kifungu cha 2).

2. Uchambuzi wa kina wa utendaji wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya

Sehemu hii inaangalia kwa kina jinsi Sheria ya Ulinzi na Uslama wa Taifa inavyotekelezwa katika ngazi ya wilaya. Kwa sababu Sheria hii haikujumuisha taarifa muhimu za utendaji wa kamati ya wilaya, wajumbe wa kamati walidodoswa ili kupata uhalisia wa nafasi yao katika mfumo wa uwajibikaji na usimamizi wa mabaraza haya ya ulinzi na usalama.

2.1. Kutekeleza majukumu ya Kikatiba

Utafiti huu umegundua kuwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zinatekeleza majukumu yao kwa dhati na umakini mkubwa. Japokuwa kunakuwapo utofauti kidogo kati ya kamati hizi kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao. Kamati zote zilizododoswa huandaa mara kwa mara mipango na mikakati pia kutathmini ripoti za hali ya ulinzi na usalama katika wilaya zao, kama inavyoelekezwa na Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa (NSC Act). Kwa kawaida mipango, mikakati na tathmini hizi huwasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa husika. Ripoti hizi husambazwa kwa wajumbe kutoka wilaya zingine kufuatia sifa zao za kuwa wajumbe wa kamati za ulinzi na usalama. Hata hivyo, vyombo vingine, ambavyo ni Idara ya Usalama wa Taifa (TIS), Ofisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), Sekretarieti ya Maadili ya Mkoa na TAMISEMI[22], hupokea maelekezo ya utekelezajia.

Ripoti za mipango, mikakati na tathmini zinaandikwa kulingana na taarifa zilizopokelewa na wajumbe wa kamati ya wilaya kutoka mamlaka ya ngazi ya kata na vijiji pia kupitia mpango wa polisi jamii na vikao vya wananchi. Hata hivyo taaarifa hizi ni lazima zipitishwe na mkuu wa mkoa. Baada ya kuridhiwa na Mkuu wa Mkoa Kamati

22 TAMISEMI ni mamlaka ya uangalizi wa Serikali za Mitaa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu

ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ugawa majukumu ya kiutekelezaji kulingana na idara. Mfano, ni jinsi Kamanda wa Polisi wa wilaya alivyopewa jukumu la kuandaa mikakati ya kukabiliana na uvunjifu wa sheria siku ya Krismasi na Mwaka Mpya.

Kamati pia inajukumu la kupanga, kuratibu na kutoa maelekezo ya jinsi ya kukabiliana na majanga na uhalifu mkubwa katika mkoa. Kamati zote zilizohojiwa isipokuwa moja zilikiri kuwahi kushughulika na uhalifu katika wilaya zao. Makosa ya jinai yaliyo tajwa sana ni uuwaji (hususan wa vikongwe wanaodhaniwa ni wachawi), ubakaji na kwa kiasi fulani migogoro ya ardhi.[23] Maelekezo na miongozo hutolewa na kamati za ulinzi na usalama na kuhakikisha inafuatilia hatua zilizochukuliwa. Hii uhusisha, kuundwa kwa kamati ndogo, kuchukua hatua za kiutawala kwa kutoa elimu kupitia mikutano na vyombo vya habari, kufanya ukaguzi, kufuatilia na kutathmini (ripoti zinatolewa).

Kamati zote za Ulinzi na Usalama za Wilaya zimekuwa zikibainisha matatizo ya kijamii na kiutawala ambayo kamati zinapaswa kubainisha. Rushwa imekuwa kinara na masuala mengine ya kiutawala ni mengi na yamekuwa yakitofautiana kutoka wilaya moja kwenda nyingine. Wilaya moja ilibainisha yafuatayo: afya (wagonjwa hawaridhiswi na huduma wanazopewa hospitalini); elimu (wanafunzi kupata mimba, utoro, mvutano baina ya walimu); migogoro ya ardhi (wananchi hawaridhi na fidia wanayopewa kutoka mamlaka za manispaa); na matumizi mabaya ya madaraka ikiwa rushwa. Kamati nyingine ilitaja ukosefu wa huduma za jamii (Usafiri na mafuta), utoaji huduma usiokidhi wa RITA[24], kutokufuata kwa sheria na kanuni za kazi na ajira, umeme kukatika hovyo miongoni mwa matatizo mengine.

23 Baadhi ya majibu ya madodoso yameonesha kwamba Baraza la Taifa la Usalama yanataarifa za vitendo vya uhalifu mkubwa unaotokea kwenye wilaya mbalimbali, Hii inadhihirisha kuwa, Baraza la Taifa la Usalama linataarifa muhimu juu ya matukio makubwa ya kiuhalifu kwa nchi nzima na hivyo lipokwenye nafasi nzuri ya kuandaa mkakatiwa kitaifa wa kuzuia uhalifu.

24 RITA ni Mamlaka inayojihusisha na usajili wa vizazi na vifo;

Majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama za Wilaya na Wajumbe wake kisheria

Majukumu ya kijamii na kiutawala yaliyoainishwa hapo juu hudhihirisha ukubwa na upana wa majukumu ya Kamati za Ulinzi na Usalama kiutendaji. Utambuzi na uelewa mpana wa masuala ya usalama, unaendelea kuonyesha utofauti kati ya sifa za ujumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kisheria na masuala wanayohitajika kufanya. Hili linatofautisha uelewa wa zamani kuhusu usiri katika mambo ya usalama kwa wateule wachache dhidi ya uhalisia wa kushughulika na changamoto mbalimbali za kijamii na masuala ya usalama.

Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zilizohojiwa zina mipango na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo na inaratibiwa na ofisi na taasisi mbalimbali za serikali. Hizi hujumuisha si tu Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa, wizara na idara za serilikali bali taasisi kama PCCB, TANESCO,[25] MWAUWASA,[26] TASAF,[27] TAMISEMI, TPF pamoja na Mkurugenzi wa Wilaya. Mjumuiko huu wa wadau wanaohusishwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya unasawiri changamoto mtambuka wanazoshughulika nazo. Kuhusu ufuatiliaji, ukaguzi wa magereza, hospitali na vituo vya polisi, hatua za mashauri ya rushwa, kuchukuliwa kwa hatua za kiutawala ni miongoni mwa mifano iliyotolewa katika hatua za ufuatiliaji. Uwasilishaji wa ripoti za utekelezaji kutoka taasisi hizi ni moja ya vitu vilivyotajwa na kamati.

25 Kampuni ya Kusambaza Umeme Tanzania;
26 Mamlaka ya Kusambaza Maji Mwanza Mjini;
27 Mfuko wa Jamii Tanzania

Utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya chini ya Sheria ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa (NSC Act), 2010

Katika Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa hakuna kipengele kinacholazimishwa taasisi hizi kutekeleza matakwa na maelekezo ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya. Japokuwa hakuna taarifa zilizotolewa na kamati kuhusu maelekezo yao kutotekelezwa. Kimsingi, utekelezaji wa majukumu kwa taasisi zilizotajwa hapo juu zinasaidia kamati kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa ufanisi. Japokuwa kutokuwepo kwa kifungu cha sheria cha aina hii kinaweza kusababisha matumizi mabaya ya madaraka kwa wajumbe wa kamati. Umuhimu wake hutokea kipindi maelekezo hutolewa kwa taasisi, yaani polisi, inayohusika na kusimamia haki za binadamu, na uhuru wa wananchi. Suala la mahusiano kati ya polisi na serikali ni nyeti, hivyo mahusiano haya ni vyema yakabainishwa, ya dhibitiwe na kusimamiwa katika ngazi zote. Jukwaa la Haki na Usalama limetoa andiko lenye mapendekezo ya jinsi ya kushughulika na hili katika ngazi ya kitaifa.[28] Katika ngazi ya wilaya, sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa ni lazima ijumuishe kifungu hiki ili kuhakikisha maelekezo ya kamati yanatekelezwa kwa kuheshimu uhuru na uwezo wa taasisi kufanya majukumu yake bila upendeleo.[29]

Pia, tuliziuliza kamati kuhusu wajibu wao wa kisheria katika kutathmini na kufuatili hali ya maeneo ya kimkakati ambayo ni chakula, mafuta na madawa. Kamati zote zimekuwa zikifanya kazi hii mara kwa mara. Kamati zote za Ulinzi na Usalama za Wilaya, wakati wa mahojiano (Desemba 2016) zimethibitisha kufanyika kwa tathmini ndani ya mwezi mmoja mpaka mitatu na zilionyesha mpango wa miezi mitatu ya kwanza kwa mwaka 2017. Hili linaonyesha umuhimu wa usalama wa hali ya chakula.

28 "Jeshi la Polisi na Serikali Kuu Tanzania: Muundo Madhubuti" http://bit.ly/2jb3vpO;

29 kwa maelezo zaidi juu ya mamlaka, uhuru na ueledi wa Polisi soma jarida lililotajwa hapo juu.

2.2. Utendaji wa Siku hadi siku

Ili kupata na kutathmini hatua zinaongoza shughuli za Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya dodoso liliweka kipengele mahususi ili kufahamu shughuli za kila siku za kamati. Karibu kamati zote zilionyesha ufanano katika namna ya utendaji kazi, chakushangaza ni kuwa katika Sheria ya Ulinzi na Usalama wa taifa hakuna mwongozo na kanuni zozote zilizotungwa.

Kwa ujumla kamati hizi hukutana mara moja kwa mwezi, na mara tu dharura inapotokea na huweza kukaa mpaka mara tatu. Vikao hufanyika katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya, japo mara nyingine huweza kufanyika eneo lililo karibu na tukio. Kamati moja ina utaratibu wa kufanya vikao kwa mzunguko katika kila taasisi ambazo zina wajumbe. Taarifa ya itokanayo na kikao iliyoandaliwa na Katibu Tawala wa Wilaya husambazwa kwa wajumbe wa kamati na wakati mwingine kwa taasisi ambazo kisheria si wajumbe ambazo ni TAKUKURU, Mkurugenzi wa Wilaya.

Kamati pia huwaalika wataalamu, wawakilishi kutoka taasisi binafsi, au taasisi za serikali kuhudhulia katika kikao cha Baraza la Ulinzi na Usalama. TAKUKURU, TANESCO, Wakala wa Misitu, Mtendaji wa Kata, na Mkurugenzi wa Wilaya ni miongoni mwa waalikwa waliotajwa kualikwa katika vikao vya kamati. Kuhusu muundo wa kamati kisheria, wajumbe wa kamati zote, isipokuwa moja, walionyesha kutoridhishwa na muundo hivyo walishauri TAKUKURU na Mkurugenzi wa Wilaya kutambuliwa kisheria na kuwa wajumbe wa kudumu wa kamati. Kamati zingine tatu zilipendekeza Afisa Mkuu wa Usalama wa wilaya ambaye ni mtunzaji wa nyaraka zote za wilaya anapaswa kuwa katibu wa kamati badala ya Katibu Tawala wa Wilaya.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kamati zote zilizohojiwa zinaunda kamati ndogo ambazo zikikamilisha kazi zilizopewa huwasilisha ripoti kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya. Kamati hizi ndogo hazina uhuru wa kutekeleza jambo bila maelekezo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama na zinaundwa kutokana na Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa. Wajumbe wake wanaweza kujumuisha

wataalam kutoka nje ya kamati hususan masuala yahusuyo afya, kilimo na elimu. Masuala ya migogoro ya ardhi, utoro wa/na wanafunzi kuacha shule, uuzaji na ununuzi wa korosho, usambazaji wa umeme na maji; polisi jamii; na uanzishwaji wa vituo vya polisi na doria; na matukio ya mauaji; mifano hii imetolewa ili kuonyesha ni jinsi gani kamati za wilaya huweza kushughulikia mambo mengi.

Utafiti pia ulibainisha kuwa kamati za uliunzi na usalama za vijiji na kata, katika wilaya sita kati ya nane, zinafanya kazi pamoja na kuwa Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa haizitambui. Pamoja na kuwa majukumu yao hayajulikani lakini zimekuwa zikisadia kutoa taarifa kwa Kamati za Wilaya ili kuandaa ajenda za vikao. Usalama na usiri ndiyo umekuwa sababu kubwa ya kutobainisha kamati hizi kisheria japokuwa zina umuhimu. Kutokana na utata huu wa kisheria na uhitaji wa mfumo unaoeleweka wa utawala wa serikali za mitaa, Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa inapaswa kujumuisha kamati za usalama za kata na vijiji na kuainisha majukumu na wajumbe wake kulingana na Kamati ya wilaya. Mwisho, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hutoa ripoti kila mwezi na kila robo na kuipeleka kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Hata hivyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya si mara zote huwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Changomoto kubwa zilizoelezwa ni ukosefu wa fedha na vitendea kazi ambavyo ni magari, mafuta na vitendea kazi vingine ambavyo vingesadia kamati kufika katika maeneo yenye shida kiusalama. Kamati pia zimeeleza umuhimu wa kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati za vijiji na kata kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

2.3. Ukweli na Uwazi kwa Umma

Kamati zote zilizo hojiwa zilionyesha kufanana katika masuala ya ukweli na uwazi kwa umma, japokuwa Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa haijatoa uhuru huo. Hivyo kutokana na uelewa uliopo kuhusu masuala ya usalama kuwa ya kipekee na siri, hili halishangazi sana kwani mfanano wa kiutendaji kazi wa kamati za wilaya hudhirisha umuhimu wa ukweli na uwazi.

Japokuwa kuna ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika vikao vya ulinzi na usalama, nguzo kubwa ya kazi za kamati huonekana katika vikao vya mara kwa mara kuunda na kuratibu hatua za pamoja ili kukabiliana na viatarishi vya usalama. Ni kamati moja tu inayotoa taarifa za ulinzi na usalama kwa wananchi kwa kuzingatia kuwa taarifa hiyo inaruhusiwa kutolewa kwa uuma. Kamati zingine hazifanyi hivyo, wananchi hupata taarifa hizo pale tu utekelezaji wake na taratibu za kiutawala zinapoanza. Taarifa hizi hutolewa kupitia: barua, maelekezo, mikutano ya hadhara na matangazo, radio za kijamii, pamoja na katika ofisi za serikali (e.g Ofisi ya Mtendaji wa Kata). Hii huleta uwiano kati ya usiri na uwazi, ilisema Kamati moja ya Ulinzi na Usalama.

Kuhusu upatikanaji na uwepo wa maelekezo/miongozo kwa umma ya kushughulika na uhalifu na mipango ya kushughulika na changamoto za kijamii na kiutawala kamati zilijibu “Hakuna” au “Ndiyo yenye msisitizo”. Kutokana na maamuzi ya kikao, aina ya tatizo ndiyo inaamua ni vipi umma utajulishwa kwa namna gani Kamati ya Ulinzi na Usalama itashughulika nalo. Japokuwa hakuna ufanano wa taarifa za aina gani zitolewa kwa umma kutoka wilaya moja hadi nyingine. Baadhi ya kamati zinasisitiza kutotoa taarifa za aina yeyote, zingine zikisema taarifa za ulinzi na usalama ndizo wanatoa kwa umma. Ukinzani huu unasababishwa na kutokuwepo kwa namna nzuri ya kutoa taarifa za ulinzi na usalama katika Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Taifa.

Mwisho, kuhusu upatikanaji wa ripoti za mwezi na za kila robo mwaka zinazowasilishwa kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa wananchi/umma ni kamati moja tu ndiyo ilisema inatoa taarifa hizi kwa umma na zilizobaki kusema hakuna taarifa ya ripoti hizo zilizosambazwa kwa umma.

Umuhimu wa Kuanzisha kifungu cha uwazi katika Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa (NSC Act), 2010

Sehemu ya 1.3 ya andiko hili imeangazia umuhimu wa kueleza utaratibu wa usiri katika Sheria ya Ulinzi na Usalama ambayo utaondoa mgongano baina ya vifungu vya NSC na Sheria ya Uhuru wa Kupata Habari. Sheria hii inapaswa kueleza ni taarifa ipi na ya aina gani haipaswi kutolewa na kamati za wilaya kwa umma. Wakati huo huo iweke kifungu kinachoeleza hatua za kufuata ili kutoa taarifa hizo kwa umma. Kwa kifupi, iainishe ni kwa jinsi gani, mara ngapi na kwa mfumo gani kamati itatoa taarifa hizo.

2.4. Kushughulikia Malalamiko na ripoti kutoka kwa Umma

Kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zinapaswa "kuweka mfumo utakao wasaidia watu binafsi, taasisi za umma na binafsi kuwasilisha taarifa zinazohusiana na masuala ya ulinzi na usalama wa taifa".[30] Kamati hizi zinakiri kupokea mara kwa mara taarifa za aina hii zikiwa kama ripoti au malalamiko ingawa hakuna njia rasmi za kuwasilisha taarifa hizi kwa kamati ambayo inaweza kusababishwa na kutokuwepo kwa sekretarieti ya kamati hizi.

Mara nyingi ripoti zinazofika katika kamati ni zile zilipokewa na Mkuu wa Wilaya kupitia vyanzo vyake vya taarifa. Kamati nyingi hutumia njia za mawasiliano sawa na zile za Mkuu wa Wilaya ambazo ni simu, barua, maswali na majibu katika vikao vya hadhara, kufika ofisini kwa Mkuu wa Wilaya na pia masanduku ya maoni. Pia kuna kamati mbili zinazokubali taarifa zilizotumwa kwa njia ya simu ya kiganjani ya Mkuu wa Wilaya kwa sababu inafahamika. Pia njia hizi zote za mawasiliano zimetangazwa sana kupitia njia mbalimbali kama mikutano ya hadhara, vyombo vya habari, mbao za matangazo, na ofisi za umma na binafsi.

Mkuu wa Wilaya anapoipata taarifa hii huamua namna ya kuifanyia kazi. Majibu kwa ripoti hii hutegemea sana ni ya aina gani, lakini

30 Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama, 2010, Kf. 14(3);

kutokana na uzoefu hatua za kwanza zinazofanywa na Mkuu wa Wilaya ni kuitathmini na kuiandikisha ripoti hiyo. Ripoti zinazopokelewa na kamati huunda agenda za kikao na kuwa msingi wa kuchukua hatua za kiutawala. Kwa mujibu wa utafiti ripoti hizi hujadiliwa na hatua huchukuliwa kulingana na hali iliyojitokeza.

Kamati inaweza kutoa maelekezo kwa mjumbe (mfano, polisi) au chombo kutoka nje (mfano. TAKUKURU) kuchukua hatua na mara nyingi taasisi iliyopewa jukumu hili hupaswa kutoa taarifa ndani ya muda fulani uliopangwa na kamati. Iwapo kuna haja ya kufanya uchunguzi afisa au taasisi husika inapewa jukumu la kufanya hivyo na kuwasilisha ripoti kwa kamati au mamlaka husika kwa hatua zaidi.

Kuna mambo mawili ya kuzingatia, moja kamati haziwajibiki kutoa taarifa kwa walalamikaji kuhusu hatua ilipofikia na zilizochukuliwa kuhusu malalamiko yake. Hivyo, mlalamikaji atajua kuwa ripoti yake imefanyiwa kazi kwa kuangalia utekelezaji au kutotekelezwa kwake. Pili, inavyoonekana utaratibu ulielezewa hapo juu wa kupokea malalamiko na kuyatafutia ufumbuzi sio mara zote huhusisha Kamati bali huweza kufuatiliwa na Mkuu wa Wilaya pekee. Kwa mfano Mkuu wa Wilaya anaweza kuelekeza polisi kuchukua hatua bila kuitisha kamati.

Malalamiko yanayopokelewa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ziko katika makundi matano; malalamiko binafsi, dhidi ya polisi, dhidi ya vyombo vya ulinzi, dhidi ya Utawala wa Wilaya na mengine.

Aina za Malalamiko yanayopokelewa na Kamati



Malalamiko binafsi mara nyingi uhusu migogoro ya ardhi na baina ya mtu na mtu, utafiti zaidi ulifanywa ili kubaini ni kwa sababu gani watu hupenda kupata usuluhishi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama na si mahakamaani. Utafiti wa namna hii utatoa jibu juu ya namna gani Baraza la Ulinzi na Usalama linaweza kuwa njia mbadala ya kutatua migogoro. Kamati zote zilikiri kupokea malalamiko dhidi ya polisi na kamati moja kukiri kuwa malalamiko mengi huwa ni ya polisi wasio na vyeo vya kiutawala dhidi ya wenye vyeo. Pia kamati zote zimekiri kupokea malalamiko dhidi ya vyombo vingine vya ulinzi kama mgambo, askari wa huduma saidizi (Idara ya Misitu) na sungusungu. Malalamiko dhidi ya maafisa katika utawala wa wilaya pia ulibainishwa na kamati. Na zaidi imegundulika kuwa kamati zimekuwa zikishughulika na malalamiko mbalimbali kutoka kwa umma dhidi taasisi za umma na binafsi kama AMCOS[31], Mahakama (kukaa na mashauri muda mrefu), hospitali (huduma duni), RITA, na Maafisa Watendaji wa Kata. Malalamiko mengine ni ya ujumla ambayo yanalenga ukosefu wa ajira au miundombinu mibovu.

31 Vyama vya Kilimo na Masoko

3. Uwezo wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya Kiuwajibishaji na Kiusimamizi

Ni dhahiri kwamba Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zinatekeleza majukumu makubwa ya usimamizi katika taasisi mbalimbali za umma, ikiwa ni pamoja na polisi na vyombo vinavyofanya kazi za ulinzi. Hata hivyo, jukumu la uwajibikaji la Kamati sio kuchukua malalamiko, kufanya uchunguzi na kutafuta suluhu, bali ni kuelekeza na kuratibu miitikio ya mashirika kwa malalamiko, na kufanya ufuatiliaji. Lakini, utaratibu huu sio rasmi, kwa kuwa hakuna sheria inayotoa muongozo wa kupokea na kushughulikia malalamiko na kutoa taarifa kwa umma.

Kwa kuweka maanani uhaba wa rasilimali kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, uwezo wake wa kuwajibisha ofisi za umma ikiwemo polisi ni wa kushangaza. Ili kuogeza uwezo wa Kamati hizi, Sheria ya Usalama wa Taifa inapaswa kuboreshwa ili kurasimisha kazi za usimamizi za Kamati. Kanuni chini ya Sheria hii zinapaswa kuandalia na kuainisha kwa kina kazi za Kamati hizi.

Zifuatazo ni masuala muhimu ya kuzingatiwa katika sheria na/au kanuni:

- Uwezo wa kujitegemea katika kupokea malalamiko kama Kamati na sio Mkuu wa Wilaya;
- Mfumo wa kuandikisha malalamiko;
- Mfumo wa kutathmini malalamiko;
- Utaratibu wa kushughulikia malalamiko wakati wa vikao vya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya;
- Utaratibu wa kutoa kazi na majukumu kwa wajumbe wa Kamati kwa ajili ya kuchunguza na/au kutafuta ufumbuzi wa malalamiko;
- Utaratibu wa kufuatilia uchunguzi na/au kutafuta suluhu ya malalamiko utakaofanywa na wajumbe husika wa Kamati;
- Utaratibu wa kuhakikisha mlalamikaji anapewa taarifa ya maendeleo ya malalamiko yake;
- Kulinda utambulisho wa mlalamikaji kwa baadhi ya

malalamiko (hususan katika malalamiko yanayotolewa thidi ya polisi);

- Mfumo wa kuweka kumbukumbu za malalamiko kama idadi ya malalamiko, malalamiko yaliyofanyiwa tathmini, uchunguzi, kupatiwa ufumbuzi na hatua zilizo chukuliwa; na
- Wajibu wa Kamati za Ulinzi na Usalama kuwasilisha ripoti kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Kamati za Ulinzi za Usalama za Taifa ili kusaidia kuboresha utoaji wa huduma za umma pamoja na kuzingatia usalama katika ngazi za kimkoa na kitaifa.

Kiutendaji, ni muhimu kwa Kamati kuwa na sekretarieti ya kujitegemea ili kuimarisha mamlaka ya kisheria iliyonayo na kupunguza utegemezi wake kwa Mkuu wa Wilaya na wajumbe wengine wa kamati katika kupokea malalamiko/taarifa na kuyaleta chini ya usimamizi wa Kamati. Pia, inaonekana sahihi kwa kamati ya kudumu kuanzishwa ili kufuatilia malalamiko na kuratibu hatua za ufuatiliaji za Kamati.

Kimajukumu, ina shauriwa kutengeneza taratibu tofauti za kutoa na kupokea malalamiko dhidi ya taasisi mbalimbali za serikali ili kukabiliana na changamoto na hatari zitakazojitokeza hasa, malalmiko yote yanayotakiwa kupewa uzito sawa. Kwa mfano, Kamati zinatakiwa kufanya mchakato bila ulazima wa kutoa utambulisho wa mlalamikaji. Pia, Kamati za Ulinzi na Usalama ambapo ni muhimu kufanya hivyo, zinazo jukumu la kuwa kiungo kati ya mfumo wa ndani wa usimamizi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG). Vivyo hivyo aina ya uhusiano huu, unapaswa kuelezewa wazi ili kuboresha utendaji. Kwa mfano, inashauriwa kwamba mlalamikaji anapaswa kuelekezwa kwa chombo cha usimamizi wa malalamiko ndani ya jeshi la polisi na wakati huo, nakala ya malalamiko inapaswa kupelekwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa usimamizi wa ziada.

Hivyo, watengeneza sera wanapaswa kuhamasishwa kufanya utafiti zaidi kuhusu utendaji kazi wa Kamati za Ulinzi na Usalama na kurasimisha kazi za usimamizi kwa mujibu wa mapendekezo

yaliyotolewa katika utafiti huu.

Ili kuboresha na kuendeleza uwezo wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kusimamia uwajibikaji, mapendekezo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa na watunga sera.

Mfumo wa Kisheria

1. Ni muhimu sheria kurasimishwa na kupitishwa chini ya Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa ya mwaka 2010, ili kuhakikisha uendeshaji wa mahitaji yake na kutoa mwongozo kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya hivyo, kuweka usawa wa utekelezaji wa sheria.

2. Mapendekezo yaliyo orodheshwa hapa chini, yaingizwe kwenye sheria au katika kanuni zilizoundwa chini ya sheria hii.

Muundo wa Uendeshaji

1. Marekebisho ya Sheria hii yanatakiwa kufanywa ili kuwezesha kuundwa kwa Sekretarieti ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya. Sekretarieti hiyo, inapaswa kujumuisha Katibu Tawala wa Wilaya, Afisa Usalama wa Wilaya na angalau mjumbe wa kudumu wa huduma za Sekretarieti ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya.

2. Sekretariet inapaswa kuwa na anuani ya kudumu ya eneo/ofisi zake. Na kupatiwa jukumu la kupokea na kuweka kumbukumbu za malalamiko.

3. Ujumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya unatakiwa kujumuisha idara na ofisi zingine muhimu kama Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED).

4. Kamati za Ulinzi na Usalama za Vijiji na Kata zinapaswa kutambulika na Sheria ya Usalama wa Taifa, 2010 ikiwa ni pamoja na kuainisha vyema muundo, majukumu na mamlaka yake na uendeshaji wake chini ya kanuni ya sheria hii.

5. Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama wanapaswa kulipwa

posho ili kuboresha uwajibikaji na utendaji wa kamati.

Uwezo ulioimarishwa

1. Wilaya zinatakiwa kutoa fedha kwa ajili ya matumizi ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wiliya katika kuimarisha ulinzi na kugharamia vitendea kazi husika kama usafiri na mafuta.

2. Kanuni za Sheria ya Usalama wa Taifa zinapaswa kuweka bayana ushirikiano wa kitendaji kati ya asasi za kiraia na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ili kujenga uwezo na ufahamu kuhusu haki za binadamu na utawala bora.

3. Ni muhimu kuongeza katika Sheria hii, kifungu kinachoelekeza, kwamba taasisi ya serikali au ofisi, iliyoagizwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kufanya kazi au kuchukua hatua, inayo wajibu wa kujiondoa kutoka katika wajibu wa kutekeleza agizo husika, iwapo utekelezaji wa agizo utakwamisha uhuru wa taasisi au uadilifu.

Uwajibikaji na Uwazi kwa Umma

1. Sheria ya Usalama wa Taifa ya 2010 pia, inapaswa kufanyiwa marekebisho kubadilisha kifungu cha usiri kwa kuweka kifungu kinachoendana na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya 2015. Hii, itaondoa utata wowote kuhusu taarifa za aina gani zinaweza au haziwezi kutolewa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya.

2. Kifungu cha utoaji wa taarifa za kiusalama kinatakiwa kuendana na kanuni ya utoaji taarifa ikifafanua, ni mara ngapi na kwa namna gani taarifa inatakiwa kutolewa na Kamati.

Jukumu la Usimamizi

1. Sheria na kanuni zinapaswa kurasimisha jukumu la usimamizi la Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kwa kutoa:

    a) Uhuru na uwezo wa kupokea malalamiko kama Kamati na sio Mkuu wa Wilaya;

    b) Hatua za kufuatwa kwa ajili ya kutoa malalamiko;

        i. Sheria zieleze bayana ni nani anaweza kutoa

malalamiko ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata nafasi.

ii. Utaratibu wa kusajili malalamiko ujulikane kwa wananchi (mfano, ni nani anahusika na kuingiza taarifa katika kumbukumbu, nani anapaswa kutunza kitabu cha kumbukumbu na nani anajukumu la kuwasilisha malalamiko kwa ajili ya kufanyiwa tathmini n.k);

iii. Mtoa malalamiko apewa namba ya lalamiko inayofanana na namba iliyoandikishwa kwenye kitabu maalumu cha kumbukumbu za serikali.

c) Mfumo wa kutathmini malalamiko yanayotolewa:

i. Kuanzisha Kamati ndogo ya kudumu kwa ajili ya kutathmini malalamiko.

ii. Kuwekwa utaratibu wa kuendesha Kamati ndogo chini ya kanuni zilizotengenezwa na Sheria.

iii. Mlalamikaji kupewa taarifa baada ya tathmini ya lalamiko alilolipeleka katika kamati endapo halikidhi vigezo vya kufanyiwa kazi na kamati.

d) Kuweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko katika Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya;

i. Kuweka mfumo wa uandikaji na usomaji wa mitasari ya vikao vya kamati.

ii. Kuainisha utaratibu wa kufuatwa katika kufanya maamuzi katika vikao vya kamati, mfano, kupiga kura au Mkuu wa Wilaya atafanya maamuzi kutokana na maoni yaliyotolewa na wanakamati.

e) Utaratibu wa kutoa kazi na majukumu kwa wanachama wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kwa ajili ya kuchunguza na/au kutafuta suluhisho la malalamiko;

f) Utaratibu wa kufuatilia uchunguzi na/au kutoa suluhu ya malalamiko unaofanywa na wajumbe wa kamati husika;

g) Mfumo wa kumhabarisha mlalamikaji kuhusu ufuatiliaji wa malalamiko yake aliyowasilisha;

h) Mfumo wa kuweka kumbukumbu kuhusu malalamiko (idadi ya malalamiko yaliyopokelewa, kutathminiwa, kuchunguzwa, kupatiwa ufumbuzi na kuchukuliwa hatua; na

i) Wajibu wa Kamati za Ulinzi na Usalama ya Wilaya kuwasilisha ripoti kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Kamati za Ulinzi za Usalama za Taifa ili kusaidia kuboresha utoaji wa huduma za umma pamoja na kuzingatia usalama katika ngazi za kimkoa na kitaifa.

j) Utaratibu maalum kwa ajili ya kushughulikia malalamiko yanayotolewa dhidi ya polisi:

    i. Mlalamikaji anatakiwa kuwa na uhuru wa kutojulikana;

    ii. Baada ya kufanyiwa tathmini, malalamiko yanatakiwa kufikishwa kwenye Kitengo cha Ndani cha Malalamiko cha Jeshi la Polisi; na pale inapobidi, nakala ya malalamiko inatakiwa kupelekwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG).

REJEA

Sheria na vitabu

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Sheria ya Uhuru wa Kupata Taarifa ya 2015.

Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa ya 2010.

"Police Accountability: Too Important to Neglect, too Urgent to Delay", *Commonwealth Human Rights Initiative*, 2005;

"Jeshi la Polisi na Serikali Kuu Tanzania: Muundo Madhubutis", *Haki na Usalama*, 2016, kinapatikana http://bit.ly/2jb3vpO;

Kiambatisho I: Dodoso kwa Kamati za ulinzi na usalama za wilaya

KAMATI ZA ULINZI NA USALAMA ZA WILAYA DODOSO

Jina (Si lazima): _____
Nambari ya Simu (Si lazima):_____
Barua Pepe (Si lazima): _____
Jina la Wilaya: _____

Jinsia: ☐ Mme ☐ Mke

1. Mara ngapi Kamati huwa inakutana?
- 1-3 mikutano kwa mwezi
- Mara moja kwa mwezi
- Mara moja kwa miezi mitatu
- Mara moja kwa miezi sita
- Wakati inapohitajika

2. Ni eneo gani mikutano ya Kamati hufanyikia?

_____
_____
_____

3. Je, yatokanayo ya kila mkutano huandikwa na kusambazwa kwa kila mjumbe wa Kamati?
- Kawaida husambazwa
- Husambazwa Mara kwa mara
- Wakati mwingine husambazwa
- Hazisambazwi kabisa

4. Mara ngapi Kamati hualika watu wengine kuhudhuria mikutano kwa dhumuni la kutoa michango na ushauri?
- Katika kila mkutano
- Mara kwa mara
- Wakati mwingine

- Hawaalikwi kabisa

5. Je, ajenda na matokeo ya vikao vya Kamati hupatikana kirahisi kwa umma?
- Ndiyo, vyote matokeo na ajenda
- Ajenda peke yake
- Matokeo peke yake
- Hapana

6. Kama ndio, tafadhali eleza njia ambayo ajenda na matokeo hutolewa kwa umma (kwa mfano, kupitia mbao za matangazo, magazeti, matangazo kwa umma kwa kutumia redio, intaneti au njia nyinginezo)?

_____
_____

7. Je, kamati ndogo zimewahi kuundwa kwa dhumuni la kufanya kazi maalum?
- Ndiyo
- Hapana

a. Kama ndiyo, kamati ndogo ngapi zimeundwa na majukumu yake ni yapi?

_____
_____

8. Je, Kamati imeandaa mipango na mikakati kwa ajili ya ulinzi na usalama?
- Ndiyo
- Hapana

a. Kama ndiyo, taasisi gani zimepewa mikakati na mipango hii?

_____
_____
_____

9. Je, Kamati imeandaa ripoti za tathmini za hali ya ulinzi na usalama katika wilaya?
- Ndiyo

- Hapana

a. Kama ndiyo, ripoti hizi zimefikishwa kwa taasisi gani?

_____

_____

10. Kuna uhalifu wa kiwango kikubwa katika Wilaya yako?
- Ndiyo
- Hapana

a. Kama ndiyo, tafadhali orodhesha

_____

_____

_____

b. Kamati yako imetoa miongozo au maelekezo ya namna ya kukabiliana na uhalifu huu?
   - Ndiyo
   - Hapana

c. Kama ndiyo, hii miongozo au maelekezo inapatikana kwa umma?
   - Ndiyo
   - Hapana

d. Tafadhali toa maelezo kwa kifupi kuhusu ufuatiliaji wa maelekezo au miongozo hii iliyotolewa

_____

_____

_____

11. Je, kamati imeainisha changamoto za kijamii na kiutawala zinazohusiana na suala la usalama katika Wilaya?
- Ndiyo
- Hapana

a. Kama ndiyo, tafadhali orodhesha,

_____

_____

_____

b. Je, kamati ina mikakati ya kukabiliana na hizi changamoto?
   - Ndiyo
   - Hapana

c. Kamati imeshirikisha mamlaka zozote mikakati hii kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki
   - Ndiyo
   - Hapana

d. Mamlaka gani zimeshirikishwa kwa kupewa taarifa kuhusu hili?
   _____
   _____
   _____

e. Tafadhali toa ufafanuzi wa jukumu la ufuatiliaji lililofanywa na mamlaka hizi?
   _____
   _____
   _____

f. Mikakati hii inapatikana kirahisi kwa umma?
   - Ndiyo
   - Hapana

12. Kamati inatathmini na kufuatilia hali ya maeneo ya kimkakati ya chakula, madawa na mafuta?
   - Muda wote
   - Mara kwa mara
   - Wakati mwingine
   - Hafuatii kamwe

g. Mara ya mwisho kufuatilia ilikuwa lini?
   _____

13. Je, Kamati huwasilisha ripoti za robo mwaka kwa Kamati ya Taifa

ya Usalama?
- Ndiyo
- Hapana

a. Je, hizi ripoti za robo mwaka zinapatikana kwa umma?
   - Ndiyo
   - Hapana

14. Je, Kamati hupokea taarifa na/au ripoti za watu binafsi, umma na/ au taasisi binafsi kuhusu masuala ya ulinzi na usalama wa taifa?
- Mara kwa mara
- Wakati mwingine
- Haijawahi

15. Je, kuna njia rasmi ya kuwasilisha aina hii ya taarifa?
- Ndiyo
- Hapana

b. Kama ndiyo, tafadhali eleza kwa kifupi kuhusu njia hizi:

_____
_____
_____

c. Je, njia hizi zinajulikana na kwa umma?
   - Ndiyo
   - Hapana

d. Tafadhali fafanua namna ambavyo taarifa hizi zimetangazwa kwa umma:

_____
_____
_____

16. Ni aina gani ya hatua ambazo Kamati huchukua baada ya kupokea taarifa na/au ripoti kutoka watu binafsi, umma na/au taasisi binafsi?

_____
_____
_____

17. Je, Kamati inapokea malalamiko yoyote kutoka kwa umma?
- Ndiyo
- Hapana

a. Kama ndiyo, ni malalamiko ya asili gani?
   - Malalamiko binafsi (migogoro ya ardhi n.k)
   - Malalamiko dhidi ya polisi
   - Malalamiko dhidi ya vikosi vya usalama
   - Malalamiko dhidi ya utawala wa Wilaya
   - Malalamik mengineyo (tafadhali ainisha):

_____

18. Unaridhika na muundo wa Kamati?
   - Ndiyo
   - Hapana

b. Kama hapana, unayo mapendekezo yoyote kuhusu muundo wa Kamati?

_____
_____
_____

19. Kwa mtazamo wako, unadhani itakuwa msaada kwa kazi za Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa iwapo Kamati za Vijiji/Kata zitaundwa?
   - Ndiyo
   - Hapana

a. Tafadhali elezea kwa nini:

_____
_____
_____

20. Kamati inakabiliwa na changamoto gani?

_____
_____
_____

21. Kuna jambo lolote ungependa kuona linafanyiwa maboresho katika kazi za Kamati? Kama ndiyo, elezea:

_____
_____
_____

Kielelezo II: Sura za wilaya[32]

Ramani ya Kamati za Ulinzi na Usalama zilizohojiwa



32 Takwimu za dadi ya watu na uwezo wa kusoma na kuandika inatolewa na kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012 ya Idadi ya Watu na Makazi (PHC);

Wilaya ya Kibiti

Idadi: hakuna taarifa.[33]

Jiografia: Kaskazini, Wilaya ya Kibiti imepakana na Wilaya za Kisarawe na Mkuranga, upande wa Mashariki na Bahari ya Hindi, Kusini na Wilaya ya Rufiji na Magharibi imepakana na Mkoa wa Morogoro.

Shughuli kuu za kiuchumi: Kilimo, uvuvi, biashara ndogo ndogo na ajira za kulipwa.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: hakuna taarifa.[34]

Manispaa ya wilaya ya Lindi

Idadi ya watu: 78,841.

Jiografia: Eneo la kilomita za mraba 7,846. Manispaa ya Wilaya ya Lindi imegawanyika katika Kata 18 za: Ndoro, Makonde, Mikumbi, Mitandi, Rahaleo, Mwenge, Matopeni, Wailes, Nachingwea, Rasbura, Mtanda, Jamhuri, Msanjihili, Mingoyo, Ng´apa, Tandangongoro, Chikonji, Mbanja. Upande wa Mashariki Wilaya imepakana na Bahari ya Hindi, na kuzungukwa na Wilaya ya Lindi Vijijini upande wa Kaskazini, Kusini na Magharibi.

Shughuli kuu za kiuchumi: Uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara ya chumvi.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 72.7%

Wilaya ya Nyamagana

Idadi ya watu: 363,452.

Jiografia: Nyamagana ni miongoni mwa Wilaya saba za mkoa wa Mwanza. Pamoja na Wilaya ya Ilemela zinatengeneza Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Jiji la Mwanza lina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 1327; kati ya hizi kilomita za mraba 900 (68%) ni maji na kilomita za mraba 427 (32%) ni nchi kavu. Nyamagana ina Kata 12.

33 Wilaya ya Kibiti imeanzishwa hivi karibuni hivyo hakuna takwimu zilizopo za sensa;

34 See above.

Main economic activities: Kilimo, uvuvi, zao la chakula, biashara kubwa na ndogo ndogo, ufugaji, na ajira rasmi.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 93.1%

Wilaya ya Rufiji (Utete)

Idadi ya watu Population: 217,274.

Jiografia: Wilaya hii, ina takriban kilometa za mraba 4,500. Kiutawala, ina Tarafa sita na Kata 19 zilizogawanywa katika vijiji 94 pamoja na vitongoji 385.

Shughuli kuu za kiuchumi: Kilimo, uvuvi, biashara ndogo ndogo na ajira za kulipwa.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 63.3%

Wilaya ya Uyui

Idadi ya watu: 396,623.

Jiografia: Wilaya ya Uyui ina kilomita za mraba 13,453. Maeneo mengi yakiwa katikati ya mkoa wa Tabora, na kuzungukwa na Halmashauri ya Manisapaa ya Tabora. Upande wa Kaskazini, wilaya imepakana na Wilaya za Igunga na Nzega, Wilaya ya Sikonge upande wa Kusini, Wilaya ya Urambo upande wa Magharibi na upande wa Mashariki, Wilaya ya Iramba.

Shughuli kuu za kiuchumi: Kilimo, uvuvi, zao la chakula, biashara ndogo ndogo, ufugaji, na ajira rasmi.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 49.6%

manispaa ya wilaya ya Tabora

Idadi ya watu: 226,999.

Jiografia: Eneo la Wilaya ni kilomita 1,092 za mraba. Manispaa ya Tabora ni moja wapo ya Wilaya saba za mkoa wa Tabora. Wilaya inapakana na wilaya ya Uyui katika pande zote isipokuwa eneo dogo la Kaskazini ambako inapakana na wilaya ya Nzega. Shughuli za kiutawala ziko chini ya mkoa wa Tabora.

Shughuli kuu za kiuchumi: Kilimo, biashara ndogo ndogo, viwanda vya jadi vya kazi za mikono, ufugaji, ufugaji nyuki na kazi za nyumbani kama kupika, usafi na uangalizi.
Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 84.7%

Wilaya ya Nzega

Idadi ya watu: 502,252.
Jiografia: Eneo la Wilaya ni kilomita 6,961 za mraba. Kiutawala, Wilaya ya Nzega imegawanyika katika tarafa 4, kata 37 na jumla ya vijiji 151 na vitongoji 1,010 vilivyogawanywa bila usawa. Tarafa ya Nyasa Division inachukua takriban 33% ya jumla ya eneo la wilaya ikifuatiwa na tarafa ya Puge yenye takriban 22.9%. Tarafa ya Mwakalundi ndiyo yenye sehemu ndogo kabisa ya ardhi ikichukua asilimia 21.5 tu ya ardhi nzima. Tarafa ya Bukene inachukua asilimia 22.6 ya eneo zima la ardhi.

Shughuli kuu za kiuchumi: Kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo, na ufugaji nyuki.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 56.1%

Wilaya ya Kaliua

Idadi ya watu: 393,358

Jiografia: Eneo la Wilaya ni kilomita za mraba 14,050 ambazo ni takriban asilimia 19% ya eneo zima la mkoa wa Tabora. Ardhi ya kulima ni kilomita za mraba 1,966, ambazo kilomita za mraba 1,500 ndizo zinazolimwa kwa mwaka. Ardhi iliyobaki ya kilometa za 12,084 (86%) za mraba ni hifadhi ya misitu, nyasi na vyanzo vya maji. Upande wa Mashariki Wilaya inapakana na Wilaya za Urambo na Uyui, Wilaya za Mpanda and Mlele upande wa Kusini, na Wilaya za Uvinza na Kibondo (mkoa wa Kigoma) upande wa Magharibi. Na upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya za Ushetu (mkoa wa Shinyanga) na Bukombe (mkoa wa Geita).

Shughuli kuu za kiuchumi: Ufugaji, kilimo, biashara ndogo ndogo, na ufugaji nyuki.

Kiwango cha kusoma cha watu wazima: 52.1%

HAKI NA USALAMA

JUSTICE AND SECURITY FORUM

Kimeandaliwa na:

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	Chama cha Wanasheria Tanganyika	Taasisi ya Haki za Binadamu ya Jumuiya ya Madola
Mtaa wa Luthuli (Haki House), S.L.P 2643, Dar es Salaam, Tanzania Simu.: +255222135747/8 chragg@chragg.go.tz http://chragg.go.tz/	Mtaa wa Chato, Regent Estate, S.L.P 2148, Dar es Salaam, Tanzania Simu: +255 22 2775313 info@tls.or.tz http://tls.or.tz/	55A, Siddharth Chambers, Ghorofa ya 3 Kalu Sarai, New Delhi – 110016 Simu.: +91-11-4318 0200, Fax: +91-11-26864688 info@humanrightsinitiative.org www.humanrightsinitiative.org

Kimeandaliwa chini ya ufadhili wa:

OSIEA
THE OPEN SOCIETY INITIATIVE FOR EAST AFRICA

Open Society Initiative for East Africa
Ghorofa ya 4, Upande B,
Regent Business Park, 172
Mtaa wa Chwaku, Mikocheni
Dar es Salaam, Tanzania

978 - 9976 - 9909 - 4 - 2